**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA ULANGA**

**Shule ya Sekondari Kwiro**
**S.L.P 06**
**MAHENGE/ULANGA**
**Tarehe. 2022**

**Namba za simu:**

| | |
|---|---|
| **Mkuu wa shule** | **0717 653199** |
| **Makamu Mkuu wa Shule** | **0714 019535** |
| **Mwandamizi Malezi** | **0755 177704** |
| **Mwandamizi Taaluma** | **0656471414** |


**Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi.**
.........................................................................
**S.L.P**................................................................
.........................................................................

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KWIRO HALMSHAURI YA WILAYA YA ULANGA , MKOA WA MOROGORO MWAKA 2022/2023**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii **mwaka 2022/2023** tahasusi ya ..................Shule ya Sekondari Kwiro ipo umbali wa Kilometa mbili (2km) Magharibi mwa mji wa Mahenge. usafiri kutoka Dar Es Salaam au Morogoro ni wa basi la moja kwa moja mpaka Mahenge kampuni ya KIDINILO/AL-SAEDY nauli kutoka DAR----MAHENGE 25,000/=.. NA MORO – MAHENGE shilingi 20,000/= Usafiri wa pikipiki kutoka kituo cha basi Mahenge kwenda Kwiro shuleni unapatikana kwa nauli ya shilingi 2000/= tu.
Muhula wa masomo utaanza tarehe ........................ hivyo mwanao atatakiwa kuripoti shuleni ndani ya siku kumi na nne .

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia**

***2.1 Sare ya shule***

a) Sare ya shule hii ni suruali mbili za rangi ya dark bluu zenye malinda, zisiwe za kubana (model) au mshono wa jinsi na shati mbili nyeupe za mikono mirefu.
b) Sare ya michezo kwa shule hii ni fulana mbili na bukta mbili kwa mchanganuo ufuatao
   PCB Rangi ya bluu
   CBG Rangi ya manjano
   PCM Rangi nyekundu
   EGM Rangi nyeupe
   HGE Rangi ya kijani
   HGL Rangi ya damu ya mzee
   HGK Rangi ya kijivu

Scanned with CamScanner

c) Viatu vya shule vyeusi vya kufunga na kamba na vyenye visigino vifupi vya ngozi jozi mbili
d) Soksi jozi nne nyeusi tu
e) Mkanda wa kuvalia suruali ni mweusi wa ngozi
f) Sweta mbili za rangi ya dark bluu (zinapatikana shuleni kila sweta shilingi elfu kumi na tano(15000) yenye muhuri wa shule.)
g) Nguo za kushindia ni truct suit mbili za rangi ya dark bluu
h) Tai jozi 2 za mistari ya pundamilia zenye rangi ya dark bluu na rangi nyeupe iliyolala (zinapatikana shuleni) kwa shilingi elfu sita kila moja.(6000)
i) Raba kwa ajili ya michezo
j) Fulana (T-shirt) za rangi ya dark bluu (zinapatikana shuleni) kwa gharama ya shilingi kumi na tano kila moja(15000).

**NB:** Mwanafunzi anaporipoti shuleni awe amevaa **truck suit ya rangi ya dark bluu** na vifaa vingine vitakaguliwa siku ya kuripoti

Mwanafunzi haruhusiwi kuja na masweta yenye kofia (pull over), kofia au miwani ya jua. atakapokuja navyo vitachukuliwa na hatua kali zitachukuliwa dhidi yake.

**2.2 Ada na Michango ya Shule**

a) Ada ya shule kwa mwaka ni **shilingi 70,000/= tu,**
b) Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi/mlezi ni kama ifuatavyo
   i. Ada ya shule shilingi 35000 kwa muhula.
   ii. shilingi 15,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani
   iii . shilingi 6,000/= kwa ajili ya kitambulisho
   iv. shilingi 30,000/= kwa ajili ya taaluma
   v . shilingi 30,000/= kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi na vibarua wengine
   vi. shilingi 2,000/= kwa ajili ya nembo ya shule
   vii . Shilingi 20,000/= kwa ajili ya kutengeneza viti na meza.
   viii . shilingi 10,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza na bima ya afya .
   ix. Tahadhari 5,000/= (haitarejeshwa)

**Jumla ya ada na michango yote ni shilingi 153,000/=.** fedha hizo zilipwe kwenye akaunti ya shule **namba 21901000019 NMB** kwa jina la **Kwiro Secondary Revenue Collection** (tafadhali andika jina la mwanafunzim katika paying slip ya benki)

c) Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:
   i. Ream mbili, kwa mwaka, kwa ajili ya matumizi ya shule .
   ii. Vitabu vya masomo ya tahususi husika viwili kati ya hivyo vitakabidhiwa shuleni na kuwekwa/kuhifadhiwa maktaba (vitakaguliwa siku ya kuripoti)
   iii. Dissecting kit kwa mwanafunzi wa biolojia
   iv. Scientific calculator
   v. Godoro la sponji 2½ x 6 futi, unashauriwa kununua duka la shule.
   vi. Mashuka jozi mbili rangi ya light bluu ,blanket moja, foronya moja rangi ya light bluu na chandarua moja (vyote hivi vitakaguliwa siku ya kuripoti)
   vii. Vyombo vya chakula sahani, bakuli na kikombe (vyote vya bati au mfupa) na vitakaguliwa siku ya kuripoti
   viii. Ndoo ndogo mbili zenye mifuniko zinapatikana duka la shule.

Scanned with CamScanner

ix. Jembe, fyekeo, ufagio laini wenye mpini (soft broom) na squeezer kwa michepuo ya PCB, CBG Na PCM tu. jembe, mfagio wa buibui, fyekeo lenye mpini wa mbao, na ufagio wa chelewa wenye mpini mrefu na reki kwa michepuo ya EGM, HGE,HGL NA HGK
x. Kila mwanafunzi aje na Flat file mbili moja kwa ajili ya kutunza mazoezi na mitihani ya ndani, na moja litakabidhiwa kwa mwalimu wa malezi
xi. Mwanafunzi atatakiwa kuja na taa ndogo ya sola itakayomsaidia pindi umeme ukikatika (solata)

NB: **Kuepukana na usumbufu unaojitokeza sambamba na kuibiwa wazazi mnashauriwa kununua vifaa vyote shuleni kwani huduma za kifedha zinapatikana shuleni.**

### 3. MAKOSA YATAKAYO SABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE MARA MOJA

i. Wizi
ii. Utoro( kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa
iii. Kugoma au kuhamasisha mgomo
iv. Kutoa lugha chafu kwa walimu/walezi au kwa mmwanafunzi mwenzake na jamii kwa ujumla
v. Kupiga au kupigana
vi. Kuwa na nywele ndefu,kucha pamoja na kufuga ndevu
vii. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya
viii. Uvutaji wa sigara
ix. Uaesherati,uhusiano wa jinsia moja kuoa au kuolewa
x. Kushiriki matendo ya kihalifu, siasa na matendo mengine yoyote yanayovunja sheria ya nchi
xi. Kusababisha mimba
xii. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba zakulala wageni
xiii. Kumiliki,kukutwa au kutumia simu ya mkononi ndani na nje ya MAZINGIRA YA SHULE
xiv. Kudharau bendera ya Taifa
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiuwa au kutishia kujiuwa kama kunywa sumu na mengineyo
xvi. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi
xvii. Kukutwa bwenini wakati wa vipindi vya darasani mchana na usiku
xviii. Kutohudhuria vipindi vya dini ambavyo vipo kwa mujibu wa sheria na kanuni za shule.
xix. Kuwa nje ya uzio wa shule bila ruhusa
xx. Kujichukulia sheria mkononi kwa mwanafunzi au raia kama vile kupiga au kutoa adhabu yoyote ile kwa mwanafunzi mwenzako pasipo kuwa na kibali kutoka kwa Uongozi wa Shule
xxi. Kukutwa na silaha ya aina yoyote ile bwenini kama panga, fyekeo, jembe au mkasi wa maua
xxii. Kukutwa na kitu chochote hatarishi kinachoweza kusababisha moto bwenini kama vile vifaa vya umeme, mafuta ya taa, petrol au spirit.

**NB: Mwanafunzi haruhusiwi kuja na redio au kifaa kingine chochote kinachotumia umeme**

Scanned with CamScanner

**4. Viambatanisho na fomu muhimu**

a) Fomu ya uchunguzi wa afya **Medical examination form** ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya serikali

b) Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai

c) Fomu ya mzazi/mlezi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni, kulipa ada na michango mengine pamoja na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule

d) Mzazi/Mlezi aje na namba ya simu ambayo ataungwa kwenye group la wazazi pamoja na walimu kwa ajili ya taarifa za kila siku shuleni (whatsap)

**5. Tafadhali soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**NB:** WAZAZI MNAHIMIZWA MWANAFUNZI AWAHI KURIPOTI SHULENI VINGINEVYO TAARIFA ITOLEWE MAPEMA KWA UONGOZI PIA MWANAFUNZI HATAPOKELEWA SHULENI ENDAPO ATAKUJA BILA ADA NA MICHANGO YA SHULE.

PIA MWANAFUNZI ATATAKIWA KURUDI KWA MZAZI/MLEZI WAKE WAKATI WA LIKIZO ZOTE NA SIO KUBAKI KWA NDUGU NA JAMAA AMBAO HAWAFAHAMIKI KWA UONGOZI WA SHULE.

**KARIBU SANA KWIRO SEKONDARI.**

Saini ya Mkuu wa Shule......................

Jina la Mkuu wa Shule: **JOHN A. KASHAMBA**

Muhuri wa Mkuu wa Shule

THE HEAD MASTER
KWIRO SECONDARY SCHOOL
P.O.Box 06
MAHENGE/ULANGA

Scanned with CamScanner

## STUDENT MEDICAL CERTIFICATE

To be completed by the Government Medical Officer and returned to the Headmaster of Kwiro Secondary School BOX 06 Mahenge/Ulanga.
Date……………………………

THE HEAD MASTER
KWIRO SECONDARY SCHOOL
P.O.Box 06
MAHENGE/ULANGA

**To the medical officer**

…………………………………….
…………………………………………
……………………………………………
Re……………………………………………………………………..
Please examine the student mentioned above and comment on his health by responding to the following items. Kindly put a tick or cross in front of either Yes or No
Headmaster

1. Does the student have the problem in connection with

a) Sight?..........No ( ) Yes ( )
If Yes state and recommend………………………………………………………………………………

b) Hearing?............ No ( ) Yes ( )
If Yes state and recommend………………………………………………………………

c) Speech?............. No ( ) Yes ( )
If Yes state and recommend………………………………………………………………………

TB? .......... No ( ) Yes ( )
If Yes state and recommend……………………………………………………………………………………
……

BP?......... No ( ) Yes ( )
If Yes state and recommend……………………………………………………………………………………
…

Any other disability?………… No ( ) Yes ( )
if Yes state and recommend……………………………………………………………………………………
……………………………………

What is your recommendation on the said student medical fit for studying at this school
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
………………………………………………..

Scanned with CamScanner

## UTHIBITISHO WA MZAZI/MLEZI

Mimi Mzazi/Mlezi wa ……………………………………………………………………………
Nitahakikisha mwanangu anafuata sheria, kanauni na taratibu zote kama ilivyoagizwa kwenye barua ya kujiunga na shule hii na kutimiza michango yote kwa wakati na kwa kipindi chote ambacho atasoma hapo shuleni
Jina la Mzazi/Mlezi……………………………………………………………………………

Sahihi…………………………………………….
Tarehe……………………………………………

***NB: Kabidhi fomu hii wakati wa kuripoti au usajili***

## Yah: KUTAMBUA UWEPO WA SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE

Mimi…………………………………………………………………………………wa kidato …………………..mchepuo wa…………………..ninaahidi kufuata taratibu zote kama nilivyoelekezwa na Uongozi wa shule pamoja na barua ya kujiunga niliyopewa. Nikikiuka nichukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria,kanuni na taratibu za shule ichukue

Sahihi……………………………………….
Tarehe……………………………………..

Scanned with CamScanner